

Utangulizi.

- * Mahindi ni zao kuu la chakula kwa wakulima wengi katika Mkoa wa Tabora na nchini kwa ujumla
- * Sehemu kubwa ya ardhi inayolimwa Mkoa wa Tabora uko katika muinuko wa kati ya meta 1000 hadi 1500 juu ya sawa wa bahari.
- * Una hali ya hewa ya joto kiasi na baridi kidogo mwezi Juni.
- * Mkoa huu pia hupata mvua haba, wastani wa milimita 700 hadi 1000 kwa mwaka na mtawanyiko usio sawa.
- * Wakulima wengi wa Mkoa huu hulima tumbaku kama zao lao la kipaumbele. Lakini pia hulima mahindi kwa ajili ya chakula.

Changamoto

- * Kutokana na mabadiliko ya tabianchi mara nyingine mvua huwahi au huchelewa na pengine huwa kidogo au hukatika mapema kabla ya mahindi hayajakoma
- * Wakulima wengi hupanda aina duni za mbegu za mahindi ambayo uzalishaji wake ni mdogo.

Suluhihisho

- * Kutokana na hali hii kituo cha utafiti cha TARI Tumbi kimezalisha aina mpya za mbegu za mahindi yanayokomaa mapema ,yanastahimili ukame, yanazaa sana na yanastahimili magonjwa mbalimbali.
- * Mbegu zilizozalishwa ni zile za uchavazi huru (OPV) aina mbili; T104 na T 105; na zilzodhibitiwa katika uchavushaji wake (hybrid) aina moja TH 501.



T 105

T 104

Sifa zake:-

- * Yanastawi vizuri katika ukanda wa chini na wa kati (0m –1500m asl).
- * Hustahimili ukame wa kati
- * Hukomaa mapema (wastani wa siku 104 –120)
- * Hutoa mavuno mengi , wastani wa gunia 18 kwa ekari
- * Yanakoboleka vizuri
- * Matamu kwa kuchoma, hivyo yanafaa kwa kilimo cha bustani.
- * Zina ukinzani na magonjwa mbalimbali kama; milia ya mahindi (MSV),
- * Bakajani kijivu (Gray leaf spot) na kutu ya majani (Leaf rust)



105

Sifa zake: T 104

-
- * Yanastawi vizuri katika ukanda wa chini na wa kati (0m –1500m asl).
- * Hustahimili ukame wa kati
- * Hukomaa mapema (wastani wa siku 110–125)
- * Hutoa mavuno mengi , wastani wa gunia 20 - 22 kwa ekari
- * Yanakoboleka vizuri
- * Yanapunje nene
- * Matamu kwa kuchoma, hivyo yanafaa kwa kilimo cha bustani.
- * Zina ukinzani na magonjwa mbalimbali kama; milia ya mahindi (MSV),
- * Bakajani kijivu (Gray leaf spot) na kutu ya majani (Leaf rust)

TH 501

Sifa zake;-

- * Hustawi vizuri katika ukanda wa chini na wa kati mita 800 hadi 1500 kutoka usawa wa bahari.
- * Ina ukinzani na mdudu tembo wa ghallani (Maize weevil).
- * Hukomaa kwa siku 120
- * Hutoa mavuno mengi wastani wa gunia 24 kwa ekari.
- * Yana punje nene
- * Yanakoboleka vizuri
- * Yanavumilia magonjwa; milia ya mahindi, bakajani kijivu na kutu ya majani.

Sehemu mbegu hizi zinakofaa kulimwa:

Aina hizi za mbegu za mahindi zinatafia kulimwa katika mikoa ifuatayo; Tabora, Kigoma, Shinyanga, Kagera, Geita, Simiyu, Mwanza, Morogoro, Pwani, Tanga, Arusha na Kilimanjaro na sehemu zingine zenye hali ya hewa inayofanana na ya mikoa hizi.



TH 501

19/07/2019 17:31

Jinsi ya Kulima na matunzo:

Panda mapema mvua za mwanzo

Nafasi za kupanda sm 75 x 30 mbegu moja maeneo yenye mvua za chini ya wastani.

Nafasi ya 75 x 25 kwa maeneo ya mvua za juu tya wastani .Mashimo yawe na kina cha sm 3 -5. Weka mbolea ya kupandia sm 2.5 –5 chini pembeni ya mbegu na isigusane na mbegu. Weka mbolea ya kukuzia mimea ikiwa na majani 6 au baada ya siku 30 toka kupanda . Mbolea iwe umbali wa sm 5 toka mche . Palizi ya kwanza ifanyike kabla ya siku 28. Tangu mahindi kupandwa



T 104



T 105

begu hizi zinapatikana kwenye maduka ya pembejeo za kilimo au kwa maelezo zaidi maelekezo zaidi wasiliana na matalamu wa kilimo aliye karibu nawe. Au ulizia ofisi ya kilimo na mifugo ya wilaya yako.

Hitimisho:

- Mahindi yanayokomaa mapema yanaweza kui-epusha familia na njaa wakati ikitubiri yale ya muda mrefu.
- Ili kupata mavuno mengi zaidi ni muhimu kufuata kanuni zote za kilimo bora cha mahindi.
- Mahindi haya hukua haraka, hivyo ni lazima kuzingatia yafuatayo:-
 - 1 Wahi kupalilia kuondoa ushindani wa magugu kwa unyevu na virutubishi vyta mimea.
 - 2 Weka mbolea ya kukuzia siku 30 baada ya kupanda.

Taasisi ya Utafiti ya Kilimo Tanzania



**KITUO CHA TUMBI
TABORA
MBEGU MPYA ZA MAHINDI**



**YANAYOKOMAA MAPEMA
NA KUZAA SANA**

Kimeandaliwa na Kituo cha TARI –Tumbi

Mawasiliano:

Mkurugenzi wa Kituo

TARI Tumbi

S.L.P. 306

TABORA

Barua pepe: cdtumbi@tari.go.tz

Simu:+255 732 988885

Fax:+255 732 988848

Wavuti: www.tari.go.tz

Chapisho Na. 2019/3